

Mwanamume au mvulana anaweza kubakwa?

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, mtu yoyote anayelazimishwa kujamiina atakuwa amebakwa, haijalishi kama mtu huyu ni mwanamke/ msichana, mwanaume au mvulana.

Wavulana na wanaume wanaweza kubakwa na wanaume wenzao au wanaweza kulazimishwa na mwanamke kujihusisha na tendo la kujamiiana. Wanaume wanaweza kulazimisha wavulana kujamiiana kwa njia ya mdomo au njia ya haja kubwa. Kisheria hapa Tanzania tukio kama hili linajulikana kama kulawiti. Matatizo/matokeo ya kulawiti kwa wavulana ni sawa na yale yanayopatikana kwa wasichana. Wavulana wanaweza kuumizwa vibaya zaidi wakati wa kujamiiana na pia kuchanganyikiwa, kiwewe, na kwa wavulana wanapata madhara zaidi. Sheria hapa Tanzania¹² haziko wazi juu ya ubakaji kwa wavulana hata hivyo wanatambua mahusiano ya ushoga/ubasha kuwa ni kosa la jinai.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25622>